# WOKOVU KUTOKA KWENYE JAHANAMU

**Ukadiriaji:**

**Maelezo:** Njia ya wokovu kutokana na mtazamo wa Kiislamu.

**Aina:** Makala Akhera Jahanamu

**Aina:** Makala Manufaa ya Uislamu Uokoaji kutokana na Moto wa Jahanamu

**Na:** islam-guide.com

**Iliyochapishwa mnamo:** 29 Nov 2021
**Ilirekebishwa mara ya mwisho mnamo:** 18 Nov 2021

Mwenyezi Mungu amesema kwenye Kurani:

***"Hakika wale walio kufuru, na wakafa hali ni makafiri haitakubaliwa kutoka kwa yeyote wao fidia ya dhahabu ya kujaza dunia nzima lau wangeli itoa. Hao watapata adhabu chungu, wala hawatakuwa na wa kuwanusuru." (Kurani 3:91)***



Kwa hivyo, maisha haya ndiyo nafasi yetu ya pekee ya kupata Pepo na kuepukana na Moto wa Jahannamu, kwa sababu mtu akifa akiwa hajaamini, hatakuwa na nafasi nyingine ya kurejea katika ulimwengu huu ili aweze kuamini. Kama Mwenyezi Mungu alivyosema katika Kurani kuhusu yatakayowapata wasioamini Siku ya Hukumu:

***"Na unge ona watakapo simamishwa kwenye Moto, wakawa wanasema: Laiti tungeli rudishwa, wala hatutakanusha tena Ishara za Mola wetu Mlezi, na tutakuwa miongoni wa Waumini!" (Kurani 6:27)***

Lakini hakuna mtu atakaye pata nafasi hii ya pili.

Amesema Mtume Muhammad,rehema na baraka za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake: “Mtu mwenye furaha kuliko wote duniani miongoni mwa wale waliohukumiwa Motoni Siku ya Kiyama atatumbukizwa Motoni mara moja. Kisha ataulizwa, ‘Mwana wa Adamu, je! umewahi kuona kheri yoyote? Umeshawahi kuona baraka yoyote?' Kisha atasema 'Hapana, kutoka kwa Mungu, Eee Mola!'"[1]

---

Rejeleo la maelezo:

[1] *Imesimuliwa katika Swahiyh Muislamu,* #2807, and *Mosnad Ahmad*, #12699.

Anwani ya wavuti ya makala hii:

https://webcache001.islamreligion.com/sw/articles/243/wokovu-kutoka-kwenye-jahanamu

Hakimiliki © 2006-2020 Haki zote zimehifadhiwa. © 2006 - 2026 IslamReligion.com. Haki zote zimehifadhiwa.